# BARAZA LA MADIWANI MANISPAA YA MOROGORO LAPITISHA BAJETI YA BILIONI 75,372,267,796.32/= KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021.



*Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro Mhe.Pascal Kihanga(katikati) akisoma sala kwa ajili ya ufunguzi wa kikao Maalum cha Baraza la Bajeti 17/2/2020 (kulia) Naibu Meya Mhe. Isihaka Sengo, na Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro Sheilla Lukuba (kushoto)*

Baraza la Madiwani Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, katika mkutano wake maalumu wa Baraza uliofanyika Februari 17,2020 , liliidhinisha na kupitisha bajeti yake ya Tshs 75,372,267,796.32/= kwa mwaka wa fedha 2020/2021.
Akizungumza na waandishi wa habari, Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Mhe. Pascal Kihanga, ameeleza kuwa katika mwaka wa fedha 2020/2021 Halmashauri inakisia kukusanya kiasi cha Tshs 8,478,799,224.32 ambapo Tsh 498,870,893.41 ni uchangiaji wa huduma za afya na Tsh 271,759,000.00 ni uchangiaji wa ada za wanafunzi kutoka katika vyanzo vya ndani na kiasi hicho ni ongezeko la Tsh 1,772,873,011.45 ambayo ni sawa na asilimia 26.43 ya

INAENDELEA UK... 07

# JUMLA YA WATOTO 32,093 SAWA NA 72.5% CHINI YA UMRI WA MIAKA MITANO WAPATA USAJILI WA VYETI VYA KUZALIWA MANISPAA YA MOROGORO .

Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, imetoa taarifa ya ujumla ya watoto 32,093 sawa na asilimia 72.5 chini ya umri wa miaka mitano waliopata usajili wa vyeti vya kuzaliwa uku Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro akisisitiza wazazi na walezi kuwaandikisha watoto wote ambao hawajaandikishwa na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa.
Taarifa hiyo imetolewa na Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Mhe. Pascal Kihanga Machi 12, 2020 ambapo ameeleza kuwa Manispaa ya Morogoro ina jumla ya watu 315,866, ambapo kati ya hao




*Mstahiki Meya Manispaa ya Morogoro Mhe.Pascal Kihanga akitoa taarifa ya usajiri wa vyeti vya kuzaliwa watoto walio chini ya umri wa miaka 5.*

INAENDELEA UK... 11

# SALAMU ZA MKUU WA WILAYA MOROGORO MHE.REGINA CHONJO

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe. Regina Chonjo, anawatakia heri wananchi na kuwaombea afya njema katika kipindi hiki cha janga kubwa la Ugonjwa wa (COVID -19) CORONA lililoikumba Dunia nzima.

Kama ilivyoada afya ni moja ya vipaumbele katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, hivyo katika kipindi hiki kigumu nacha mashaka, Mkuu wa Wilaya anawataka wananchi wote wajikinge na virusi vya CORONA kwani kila mtu akiwa makini na akifuata maelekezo ya Madaktari na wataalamu wa afya ,ugonjwa huo unazuilika kama wananchi wote wakijikinga na kukinga wengine kwa kuepuka kushikana mikono, kushika sehemu za uso, kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni mara kwa mara, kuepuka maeneo yenye msongamano au makutano ya watu wengi pamoja na kuwa makini na kujenga tabia ya kula vyakula vya moto ili kuua na kuangamiza Virusi vya CORONA .

Nina matumani kwamba kwa umoja, umakini na kumtegemea Mwenyezi Mungu pamoja na kufuata ushauri wa wataalamu wa afya na miongozo inayotolewa na Serikali kupitia Viongozi wa ngazi za Juu ugonjwa wa CORONA kwa Manispaa ya Morogoro hautaweza kutuathiri kwa kiasi kikubwa.

Aidha, Mkuu wa Wilaya, anapenda kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano, chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa kuiwezesha Manispaa ya Morogoro na kuipatia miradi ya kimkakati inayoelekea kumalizika ikiwamo Ujenzi wa Soko Kuu la Kisasa, Stendi Mpya ya Daladala, pamoja na Stendi ya Mabasi Msamvu ambayo ilishaanza kutumika kufuatia tamko lake la kuitaka LAPF kukabidhi Manispaa Stendi hiyo.

Ni matumaini ya Mkuu wa Wilaya kwa kushirikiana na Baraza la Madiwani Manispaa ya Morogoro, na Ofisi ya Mkurugenzi, kwa mwaka wa fedha 2020/2021 wataweza kutekeleza Ujenzi wa Machinjio ya Kisasa ili kuiongezea Manispaa chanzo kingine kikubwa cha mapato.


## BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti ...** **Sheilla E. Lukuba**
*Mkurugenzi Manispaa*

**Mhariri Mkuu ...** **Lilian K. Henerico**
*Afisa Habari Manispaa*

Washiriki wasaidizi

**Issa B. Issa:** *Afisa Habari Msaidizi*

**Yusuph A. Mwamba**
*Afisa Habari Msaidizi*



*mawasiliano:* *simu: 023 - 2935242*
*E-mail: info@morogoromc.go.tz*
*S.L.P 166*

*Mitandao ya Kijamii*

*Website:* *www.morogoromc.go.tz*
*youtube:* *Morogoro Manispaa TV*
*instagram:* *Manispaa ya Morogoro*
*facebook:* *Manispaa ya Morogoro*




*Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe. Regina Chonjo, akihutubia Baraza la Wazee la Manispaa ya Morogoro katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogro*

# WAZIRI JAFFO ARIDHISHWA NA KAZI ZA TARURA MANISPAA YA MOROGORO.



*Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI Mh. Selemani Jaffo(aliyevaa suti na tai) akikagua ujenzi wa mfereji wa maji katika barabara ya Nanenane Manispaa ya Morogoro.*

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI Mhe. Selemani Jaffo amewapongeza Wakala wa Barabara za Vijijini na Mjini-TARURA Manispaa ya Morogoro kwa kazi nzuri ya kusimamia ujenzi wa barabara pamoja na kutengeneza kalavati na mifereji bora yenye kuhimiri nguvu ya maji wakati wa mvua.

Mhe. Jaffo ameyasema hayo wakati wa ziara aliyofanya Machi 13, 2020 ya kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ikiwemo miundombinu ya barabara zilizopo chini ya TARURA ambapo Ujenzi wa barabara ya Nanenane ni moja ya barabara iliyotembelewa huku akiridhika na ujenzi wa mifereji kutokana na ubora na uimara .

Aidha, Waziri Jaffo ametoa angalizo kwa TARURA kuwa makini katika kuwasimamia wakandarasi wanaojenga barabara hizo ili ziendane na thamani halisi ya fedha inayotumika.

" Hizi barabara zetu tunazijenga kwa gharama kubwa, lakini baada ya miaka miwili tunawe-

INAENDELEA UK... 23

# DC CHONJO AZINDUA MAPIPA 50 YA KUBEBEA TAKA YENYE THAMANI YA SHILINGI MILIONI 591 MANISPAA YA MOROGORO.

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe. Regina Chonjo, amezindua mapipa ya kuhifadhia takataka(skip backet) 50 yenye thamani ya Tsh 591,519,500 baada ya Halmashauri kuwa imetenga bajeti ya ununuzi wa mapipa hayo kupitia fedha za mradi wa uboreshaji miji (ULGSP).



*Mkuu wa Wilaya ya Morogoro Mhe.Regina Chonjo (katikati) akikata utepe kama ishara ya uzinduzi wa mapipa 50 ya kuhifadhia taka yaliyonunuliwa na Manispaa ya Morogoro,(kushoto) ni Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro Mhe.Pascal kihanga,(kulia) ni Mkurugenzi wa Manispaa Sheilla Lukuba.*

Zoezi hilo la upokeaji wa mabaketi hayo umefanyika Januari 18, 2020, katika Viwanja vya Kata ya Mji Mkuu, ambapo aliwataka wananchi kuvitumia vifaa hivyo kwa malengo yaliyokusudiwa.

DC Chonjo alieleza kuwa Manispaa ya Morogoro, ilikuwa

INAENDELEA UK... 06

# BARAZA LA WAFANYAKAZI SIMAMIENI MISINGI YA USHIRIKISHWAJI-MKURUGENZI SHEILLA.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Sheilla Lukuba, amelitaka Baraza jipya la wafanyakazi Manispaa ya Morogoro kuhakikisha wanasimamia mambo yote ya Msingi katika utendaji wa kila siku pamoja na kutetea haki za Wafanyakazi.



*Watumishi wakionesha furaha kwa kushikana mikono kama moja ya utambulisho wa mshikamano wa Baraza la Wafanyakazi katika kikao kilichofanyika 27/1/2020*

Hayo ameyazungumza wakati wa uzinduzi wa Baraza la Wafanyakazi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro katika mkutano uliofanyika tarehe 27 Januari 2020 katika ukumbi wa mikutano Manispaa.

Sheilla amesema uzinduzi wa Baraza hilo ni mojawapo ya utekelezaji wa maagizo ya viongozi wa Serikali yenye lengo la kuwashirikisha wafanyakazi katika uongozi wa pamoja mahala pa kazi kwa mujibu wa agizo la Hayati Mhe. Rais Julius Kambarage Nyerere tamko namba 1 la mwaka 1970, pamoja na kifungu cha 73, (1) (2), (3) cha Sheria ya ajira na Mahusiano kazini namba 6/2004 na kifungu cha 14 (1) (c) cha Sheria ya Taasisi za Kazi Namba 7/2004.

Amesema Baraza hilo ni chombo kamili kinachosimamia misingi ya ushirikishwaji wa wafanyakazi kuweza kutoa na kupokea ushauri na majadiliano sehemu za kazi kwa maslahi mapana ya Halmshauri ya Manispaa ya Morogoro.

Aidha, amesema majukumu na kazi za Baraza la Wafanyakazi zimeainishwa katika mkataba unaloliongoza Baraza hilo katika kifungu namba.8 ukurasa wa 6 na kifungu namba 10 ukurasa wa 7-8 huku kila pande husika ikiwa na nakala moja kwa ajili ya kufanya rejea ya Mkataba pale inapohitajika kufanya hivyo.

"Tumefungua Baraza letu jipya la wafanyakazi, natoa rai kuwa ili Baraza liweze kusimama vyema maslahi na stahiki za watumishi ziboreshwe vizuri, pia Baraza hili linawajibu wa kuishauri Manispaa juu ya vyanzo vipya vya mapato na namna bora ya ukusanyaji mapato, sambamba na kushauriana na mwajiri juu ya ufanisi wa kazi na hatua zinazofaa kuchukuliwa ili kuhakikisha kuwa huduma zitolewazo na wafanyakazi zinaridhisha na zimo katika malengo ya Halmshauri ya Manispaa ya Morogoro na Taifa kwa ujumla" Amesema Sheilla.

Aidha, amewaambia Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi kuwa wanapokuwa kwenye vikao vya baraza wajumbe wote wanahaki sawa ya kuchangia na kutoa mawazo ya kuboresha Halmashauri katika nyanja zote muhimu hivyo amewataka viongozi na wajumbe kuhakikisha wanatoa ushauri wa uboreshaji bila kuogopa wakuu wao wa kazi (katika marejeo ya kifungu Namba



*Watumishi wakiwa wamesimama tayari kwa uzinduzi wa Baraza jipya la Wafanyakazi lililozinduliwa katika Ukumbi wa Mikutano wa Manispaa ya Morogoro.*

11.0 ukurasa . Namba 8 cha mkataba wa Baraza la Wafanyakazi)

Pia amesema wao ni wawakilishi tu hivyo lazima watambue kwamba wapo wenzao ambao

INAENDELEA UK... 09

# SALAMU ZA MSTAHIKI MEYA WA MANISPAA YA MOROGORO MHE.PASCAL KIHANGA.

Manispaa ina jumla ya kata 29 zinazounda tarafa moja ya Morogoro mjini.Aidha katika utekelezaji wa ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kipindi cha miaka minne chini ya serikali ya awamu ya tano Serikali imekuwa ikitekeleza miradi mbalimbali katika ngazi ya kata kwa lengo la kutoa huduma bora za jamii na kiuchumi kwa wananchi wa Manispaa ya Morogoro.

Kwa upande wa elimu ya Msingi wananchi wa Manispaa ya Morogoro wanaishukuru Serikali kwa kuanzisha Sera ya elimu bila malipo, Sera hii imewezesha kuongezeka kwa uandikishaji wa wanafunzi na uboreshaji miundombinu ya kufundishia na kujifunzia suala ambalo limeleta tija kubwa kwa Taifa tangu kuanza kwa mfumo wa Elimu Msingi bila malipo Desemba, 2015.

Manispaa ya Morogoro hadi kufikia Novemba, 2019 imepokea jumla ya Tshs. 5,720,278,932, Kiasi hicho cha fedha kinajumuisha Ruzuku ya uendeshaji wa Shule, Chakula kwa Wanafunzi wenye mahitaji maalum na waishio mazingira magumu na posho ya madaraka kwa Walimu Wakuu na Waratibu wa Elimu Kata.

Kwa upande wa fedha za umaliziaji wa maboma 34 kwa shule za Msingi za Manispaa ambapo jumla ya kiasi cha Tsh. 625,000,000 kilipokelewa katika kipindi cha mwaka 2015/2019, sehemu kubwa ya miradi hii imekamilika.

Manispaa kupitia shule zake ilipokea jumla ya Tsh. 100, 000, 000 milioni zilizotolewa na serikali ikiwa ni fidia kutokana na baadhi ya majengo na maeneo yanayomilikiwa na shule za msingi kutakiwa kupisha ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) ikiwa ni fidia kwa shule ya msingi Azimio na Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.

Fedha hizo zimetumika kujenga vyumba vya madarasa 5 na kukarabati vyoo vya shule hiyo..Vyumba vya madarasa ya elimu ya Msingi vimeongezeka kutoka 634 mwaka 2015 hadi kufikia vyumba 701 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 11 hivyo kupunguza changamoto ya uwiano wa madarasa kutoka 1:100 hadi kufikia 1:50 na kwa baadhi ya shule 1:45 (Mfano S/Msingi Kikundi, Misufini A na Misufini B) ,Idadi ya matundu ya vyoo imeongezeka kutoka matundu 818 mwaka 2015 hadi kufikia matundu 841 mwaka 2019, ikiwa ni ongezeko la asilimia 2.7.

Aidha kwa upande wa elimu ya

INAENDELEA UK... 15



*Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Sheilla Lukuba , akimbeba mtoto katika ziara yake ya kuwatembelea na kuwajulia hali wakina mama wajawazito katika kituo cha Afya cha Mafiga kilichopo Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro Januari 27/2020.*



*Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Mazimbu , Mhe. Pascal Kihanga (kushoto) akisoma sala katika Mkutano maalumu wa Baraza la Madiwani kujadili (Bajeti) ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kilichofanyika 18/2/2020 .*

# DC CHONJO AZINDUA MAPIPA 50 YA KUBEBEA TAKA YENYE THAMANI YA SHILINGI MILIONI 591 MANISPAA YA MOROGORO.

INATOKA UK... 03

ikikabiliwa na changamoto ya kutokuwa na Mapipa ya kuhifadhia taka ya kutosha, ambapo awali yalikuwa 30 na mahitaji ni mapipa 100.
Amesema Mapipa hayo yametumia jumla ya Shilingi Milioni 591 kila pipa likiwa na thamani ya shilingi milioni 11 na kusababisha mapipa kuwa 80 baada ya 50 kuzinduliwa.
Äidha, amesema Mapipa hayo yatagawanywa katika Masoko, maeneo yenye msongamano wa watu, maeneo yenye shughuli nyingi za kiuchumi na kijamii.
Mara baada ya Mapipa hayo kujaa taka yatakuwa yanabebwa na gari tatu za Manispaa aina ya 'Skip Loader' na kwasasa Manispaa imeagiza magari mengine 2 ya aina hiyo kwa ajili ya uondoaji wa mapipa ya taka.
"Mapipa haya yataboresha usafi wa mji kwani wananchi watakuwa na sehemu ya kuwekea /kuhifadhi taka zao kwa muda badala ya kuzitupa hovyo au kuziweka kando kando ya barabara, niwaombe wananchi tuendelee kulipa ada ya taka ya kila mwezi ili kuwezesha Kampuni / vikundi vya usafi na Manispaa yetu kuendelea kutoa huduma bora kwa Wananchi" Amesema DC Chonjo.



*Baadhi ya Mapipa yaliyonunuliwa na Manispaa ya Morogoro kwa ajili ya kuhifadhia takataka*

Amesema Morogoro ipo kati kati ya Mji Mkuu wa Makao Makuu ya Serikali Dodoma pamoja na Mji Mkuu wa kibiashara Dar es Salaam, hivyo ili Morogoro iwe Jiji kuna vigezo mbalimbali ikiwemo suala la Usafi, mandhari husika hivyo kuna haja ya kuwa wasafi.
Pia amewataka Madiwani wa Manispaa ya Morogoro kuhimiza na kusimamia usafi katika kata zao kwa kuwa wao ndio wenyeviti wa Kamati za Maendeleo ya Kata.
" Mimi nilivyofika hapa Morogoro mwaka 2016 nilikuta kambi ya kipindupindu iliyodumu kwa miaka 5, kuanzia mwezi wa 11 , 2016 kipindupindu kilikuwa ni historia kwa manispaa yetu ya Morogoro, hiyo nayo ni sababu iliyotufanya tuchelewe kuwa Jiji, navitaka vikundi vya taka viwajibike kuanzia ngazi za Mitaa na Kata na kama vitashindwa kufanya vizuri vitafutwe vyenye uwezo wa kutatua kero za taka ambapo amesema sio vyema maafisa mazingira kufika katika mitaa yote 294 " Ameongeza DC

INAENDELEA UK... 09




*Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mhe. Loata Sanare akionesha Kitambulisho cha kupigia kura mara baada ya kujiandikisha katika Daftari la kudumu la mpiga kura katika kituo cha Liti Kata ya Mlimani Manispaa ya Morogoro.*



*Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe. Regina Chonjo, (kushoto), akikabidhi kiasi cha Shilingi Milioni Moja , kwa Mwenyekiti wa Wildna Foundation, Bi. Yustina Mutafungwa kwa ajili ya kutunisha mfuko wa kuwasaidia kujiendeleza kiuchumi kwa wakina Mama wanaoishi katika kota za polisi*

# BARAZA LA MADIWANI MANISPAA YA MOROGORO LAPITISHA BAJETI YA BILIONI 75,372,267,796.32/= KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021.

INATOKA UK... 01

makadirio ya mwaka 2019/2020 ya Tsh 6,705,926,212.87.

Aidha, amesema kuwa katika mwaka wa fedha 2020/2021 Halmashauri inatarajia kupokea kiasi cha Tsh 7,483,018,572 kutoka Serikali kuu na wahisani mbalimbali kwaajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ambapo Serikali kuu inatarajia kuchangia kiasi cha Tsh 5,832,810,000 na Tsh 1,650,208,572 ikiwa ni fedha za nje.

Pia ameeleza kuwa katika mwaka wa fedha 2020/2021 Halmashauri inatarajia kutumia kiasi cha Tsh 59,410,450,000.00 kutoka Serikali kuu kwaajili ya matumizi ya kawaida ya mishahara na matumizi mengineyo ambapo matumizi kwaajili ya matumizi mengineyo yanakisiwa kuwa Tsh 2,495,867,000.00 na itapokea kiasi cha Tsh 2,495,867,000.00 ikiwa ni ruzuku ya matumizi ya kawaida na kati ya hizo Tsh 89,196,000.00 ni fidia ya vyanzo vilivyofutwa.

Akiendelea kuielezea bajeti hiyo Meya Kihanga, ameelezea mikakati iliyowekwa ni kuhakiksha mapato yanakusanywa katika mwaka ujao wa fedha , pamoja na kupitia upya mifumo ya usimamizi na ufuatiliaji wa mapato kwa kuboresha maeneo ambayo yana mapungufu,kuendelea kuwashirikisha wadau mbalimbali katika kukusanya mapato,kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kubaini mianya inayovujisha mapato,kupitia upya sheria ndogo za mapato na kutumia mifumo ya ki-electronic katika vyanzo vyote vya mapato.



*Waheshimiwa Madiwani wakifuatilia kwa umakini kikao cha Baraza cha kupitisha Bajeti ya Manispaa ya Morogoro 2020/2021.*

Amesema kuwa ili kuboresha maisha ya wakazi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Manispaa imeandaa mpango wa mwaka 2020/2021 na mpango wa muda wa kati 2020/2021 – 2022/2023 unaolenga kukuza uchumi na kupunguza umaskini na kufikia maendeleo endelevu ya kijamii, kiuchumi,na kimazingira kwa wananchi wake.

Meya Kihanga, ametanabaisha kuwa ili kutekeleza dhana nzima ya ugatuaji wa madaraka , mpango huo umeshirikisha jamii katika mpango shirikishi kuanzia ngazi ya Mtaa kwa kuzingatia vipaumbele na mahitaji halisi ya Wananchi katika maeneo yao na kujielekeza katika kutoa kipaumbele maeneo yanayoweza kutoa matokeo ya haraka yatakayosaidia ukuaji wa uchumi kwa haraka na kwa kipindi kifupi.

Ameyataja maeneo ya kipaumbele kuwa ni pamoja na kuboresha na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kuwekeza katika miradi mikubwa ya Kimkakati, kuboresha miundombinu ya Afya, na Elimu,kuboresha hifadhi ya mazingira na ukusanyaji wa taka, kuimarisha ushirikishaji wa jamii katika upangaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo, na uboreshaji wa mazingira ya wafanyabiashara wadogowadogo kwa kuwajengea masoko katika maeneo mbalimbali.

Ili kufikia malengo yaliyokusudiwa, Meya Kihanga amewataka viongozi na watendaji wote kusimamia uimarishaji wa mahusiano mazuri kati ya Serikali ,Mashirika yasiyo ya kiserikali na wadau wengine, kujenga uwezo na ujuzi kwa watumishi katika utoaji wa huduma, kuimarisha utawala bora, uwajibikaji na uwazi sambamba na kujenga uwezo kwa viongozi wakiwemo waheshimiwa madiwani na wenyeviti wa Serikali za mitaa katika kusimamia shughuli za Wananchi.



*Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Mhe. Pascal Kihanga (mbele) akifuatiwa na Mkurugenzi wa Manispaa , Sheilla Lukuba, wakiingia katika Ukumbi wa Mikutano katika kikao cha Baraza cha kupitisha Bajeti ya Fedha 2020/2021.*

Katika hatua nyingine amesema makusanyo ya mapato yameongezeka kwa asilimia 26% kutoka Bilioni 6.7 hadi kufika Bilioni 8.4 kwa mwaka sawa na ongezeko la Bilioni 1.7, jambo ambalo linaonesha njia salama ya Morogoro kuwa Jiji kwani sifa ya jiji inachangiwa na ongezeko la makusanyo ya mapato.
Aidha amesema suala la Stendi ya Msamvu kurudishwa katika mikono ya Manispaa ya Morogoro litaleta tija kwakuwa ukukusanyaji wa mapato utaongezeka kupitia kitega uchumi hicho,hivyo Halmashauri itaweza kuendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kimaendeleo.
Pia Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Sheilla Lukuba, amewashukuru wadau wote waliofanikisha bajeti hiyo zikiwemo kamati zote za kudumu za Manispaa na Serikali kuu iliyotenga kiasi hicho cha bajeti.
Aidha ameeleza kuwa Manispaa inaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa soko kuu la kisasa ambalo kiasi cha Tsh. Bilioni 10 kilitolewa na Serikali kuu na Tsh. Bilion 7 ni Mkipo kutoka Benki kuu ya Dunia kupitia mradi wa uboreshaji Miji (ULGSP).
Pia ujenzi wa stendi ya Daladala Mafiga itakayogharimu Tsh. Bilioni 5 ambapo hadi sasa umefikia asilimia 71 ya utekelezaji, sambamba na ujenzi wa stendi ya Kaloleni utaogharimu Tsh. milioni 724 na tayari Mkandarasi ameshalipwa Tsh. milioni 108 na ujenzi wa kitega Uchumu cha DDC wenye gharama ya Tsh. milioni 620.



*Viongozi mbalimbali wa Mkoa wa Morogoro katika picha ya pamoja Jiji la Dodoma mara baada ya kuwasilisha Bajeti za Halmashauri za Mkoa wa Morogoro kwa mwaka wa Fedha 2020/2021*

# MANISPAA YA MOROGORO YAUNGANA NA TASWO KUWAFARIJI NDUGU WA MAREHEMU WA AJALI YA MOTO MSAMVU.

Jumuiya ya Wataalamu wa Ustawi wa Jamii Tanzania (TASWO) kwa kushirikiana na Idara ya Ustawi wa Jamii Manispaa ya Morogoro wametembelea wajane na tegemezi wa marehemu waliofariki katika ajali ya Moto Msamvu na kuwapatia msaada wa vyakula ikiwa ni moja ya maandalizi ya maadhimisho ya siku ya Ustawi wa Jamii Duniani.
Akizungumza katika hafla hiyo iliyofanyika Machi 17,2020 katika Ofisi ya Kata ya Mwembesongo Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro , Mhe. Pascal Kihanga, amekipongeza Chama hicho kwa jitihada za kuwajali tegemezi wa marehemu kwani wamefanya jambo la kiungwana linalostahili kuigwa na jamii kwa kuwakumbuka wajane wa wahanga wa ajali ya Moto Msamvu.
Aidha ameitaka Jamii itambue umuhimu wa kukuza mahusiano baina ya watu na watu ili kuchochea ukuaji wa kiuchumi hapa nchini na kueleza kuwa Jamii isiyokuwa na matatizo ya kijamii na migogoro ya nafsi kwa mtu mmoja mmoja ni kichocheo cha ukuaji wa uchumi katika nchi yoyote.
"Nawapongeza sana TASWO Taifa kwa kuwajali ndugu zetu, kwani wengi wao wameachwa



*Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Mhe. Pascal Kihanga, akimkabidhi kiloba cha Unga mmoja ya ndugu wa marehemu aliyepata ajali ya moto Msamvu.*

INAENDELEA UK... 18

# BARAZA LA WAFANYAKAZI SIMAMIENI MISINGI YA USHIRIKISHWAJI-MKURUGENZI SHEILLA.

INATOKA UK... 04

kwa sasa wanafikia takribani 4,293, hivyo wanatakiwa kuishauri vyema Halmashauri ya Manispaa kwa manufaa ya wenzao ambao hawapo katika kikao hicho.



*Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Sheilla Lukuba, akiwa ameshikana mikono na Watumishi wa Manispaa ya Morogoro kuashiria uzinduzi rasmi wa Baraza hilo.*

Amewashukuru Wajumbe wa Mkutano wote kwa usikivu na kuwatakia majadiliano yenye tija kila mara wanapokutana katika Vikao vyao vya Baraza . Mwisho amewataka kila mtumishi na Viongozi wa Serikali kuhakikisha wanamsaidia ,Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kufanya kazi kwa mujibu wa taratibu, Kanuni na sheria kwa maslahi mapana ya Nchi.

# DC CHONJO AZINDUA MAPIPA 50 YA KUBEBEA TAKA YENYE THAMANI YA SHILINGI MILIONI 591 MANISPAA YA MOROGORO.

INATOKA UK... 06

Chonjo.

Kwa Upande wa Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogro, Sheilla Lukuba, amewataka wananchi kutotupa taka pembeni badala yake wazihifadhi taka hizo katika vyombo husika na wale watakao kaidi watapigwa faini kwa mujibu wa sheria za mazingira.

Mbali na uzinduzi wa mapipa hayo amesema pia suala la usafi liwe katika damu na sio wananchi wangoje hadi viongozi wafike ndipo wafanye usafi.

" Suala la usafi ni kama unavyooga kila siku, jinsi ya kupiga mswaki bila kusimamiwa, kwahiyo niwasihi wananchi wa Manispaa ya Morogoro naomba tufanye usafi bila kushurutishwa , kwani hata Mhe. Rais Dkt John Magufuli amewaonesha Watanzania na kulipa kipaumbele suala la usafi" Amesema Sheilla .

Naye Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Mhe. Pascal Kihanga, amesema ujio wa Mapipa ya takataka uendane na usafi wa mazingira.

Mbali na hayo, amesema kuwa suala la usafi katika masoko bado ni changamoto na hali hairiridhishi , asilimia kubwa ya wafanyabiashara wanafanya usafi katika maeneo yanayoonekana lakini katika vizimba vyao kwa chini kumekuwa kuchafu sana jambo ambalo halipendezi na linatakiwa kuchukuliwa hatua ili masoko yote yawe safi.

Aidha Meya Kihanga amewasisitiza wafanyabiashara wa Masoko yote yaliyo katika Manispaa ya Morogoro kujitahidi kufanya usafi.



*Mkuu wa Wilaya ya Morogoro (katikati) akipitia taarifa ya Mapipa ya taka .*



*Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini, Mhe. Abdulaziz Abood (kulia) akimkabidhi Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mji Mkuu, Bi. Grace Malya (kushoto), Hundi ya Shilingi Milioni Moja na Laki Nne kwa ajili ya kuendeleza ukarabati wa madarasa matatu aliyoahidi ambapo awali alitoa shilingi Milioni 3 na laki 4 kutoka mfuko wa Jimbo. Katikati ni Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe. Regina Chonjo akishuhudia makabidhiano hayo.*

# WANANCHI WA MANISPAA YA MOROGORO WAMETAKIWA KUWA MSTARI WA MBELE KATIKA UCHANGIAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO.

Wananchi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, wametakiwa kushiriki katika kuchangia maendeleo na kuachana na dhana zinazoendelezwa na baadhi ya viongozi katika Serikali wanaotoa kauli za kuwapinga wananchi kuchangia maendeleo ya miradi ya maendeleo.



*Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mhe. Loata Sanare, akizungumza na Wananchi waliofika katika ukaguzi wa mradi wa ujenzi wa vyumba vya madarsa Shule ya Msingi Nane Nane Kata ya Tungi, katika ziara yake ya kukagua miradi ya Maendeleo Kata ya hiyo.*

Hayo yamezungumzwa na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mhe. Loata Sanare , Machi 3,2020 katika ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo na kusikiliza kero za wananchi katika Kata ya Tungi .

Akizungumza na wananchi wa Kata ya Tungi, RC Sanare, amesema uhamasishaji wa kuchangia miradi ya maendeleo hususani katika elimu, miun-

INAENDELEA UK... 13

# WANAWAKE WAJASIRIAMALI IBUENI MIRADI YENYE TIJA NA INAYOTEKELEZEKA ILI MUWEZE KUREJESHA MIKOPO KWA WAKATI-RAS MOROGORO.

Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Emmanuel Kalobelo, amewataka wakina mama wajasiriamali kuibua miradi yenye tija na inayotekelezeka ili kuweza kurejesha fedha za mikopo kwa wakati kuliko kuwa na biashara ambazo haziwezi kuwapatia faida kwa wakati.

Ameyasema hayo wakati wa Maadhimisho ya siku ya wanawake Duniani yaliyoandaliwa na Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na kufanyika katika Uwanja wa mpira wa Jamhuri Machi 8, 2020.



*Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Emmanuel Kalobelo, akimkabidhi cheti cha pongezi kwa mmoja wa wadau walifanikisha Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyoandaliwa na Manispaa ya Morogoro 08/03/2020.*

Akizungumza na Wanawake waliojitokeza katika maadhimisho hayo, amesema wajasiri-

INAENDELEA UK... 13

# JUMLA YA WATOTO 32,093 SAWA NA 72.5% CHINI YA UMRI WA MIAKA MITANO WAPATA USAJILI WA VYETI VYA KUZALIWA MANISPAA YA MOROGORO.

INATOKA UK... 01



*Baadhi ya Wakina Mama wakiwa katika foleni ya uandikishaji wa Vyeti vya kuzaliwa kwa Watoto wenye umri chini ya miaka 5.*

watoto chini ya miaka mitano ni 44,472.

Amesema kuwa, awali zoezi la usajili wa vyeti vya kuzaliwa lilikuwa likitekelezwa na Ofisi za RITA ambao kwa sasa wanaendelea kusajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa kuanzia umri wa miaka mitano na kuendelea.

Amesema kuwa tangu mpango wa kusajili vyeti vya kuzaliwa kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano ulipoanza, jumla ya watoto 32,093 (sawa na asilimia 72.5) wamesajiliwa hadi kufikia tarehe 20 Februari, 2020.

Aidha amesema kuwa , kuanzia tarehe 6/12/2019 na kuendelea zoezi la usajili wa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto chini ya miaka 5 linatekelezwa na Halmashauri kupitia Ofisi za kata na vituo vya kutolea huduma za afya vinavyotoa huduma ya baba, mama na mtoto (Kliniki) ambapo vyeti hivyo vinatolewa bila malipo.

Meya Kihanga, amesema vyeti hivyo kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano vina faida kwakuwa ni utambulisho wa awali kisheria utakaomwezesha mtoto kupata haki nyingine kama kuzuia ajira ya watoto na kuwalinda na watu wanaokinzana na sheria, kummsaidia mtoto kuandikishwa shule za Msingi na Sekondari,ni kitambulisho cha msingi ili kupata kitambulisho cha Taifa, kuwawezesha wanafunzi kujiunga na vyuo na elimu ya juu na kupata mikopo ya elimu ya juu pamoja na kumsaidia kupata hati ya kusafiria ( Passport).

Amesema miongoni mwa vitu muhimu vya kwenda navyo wazazi /walezi katika kituo cha usajili ni pamoja na nakala ya kadi ya kliniki au tangazo, barua ya mwenyekiti wa Mtaa, cheti cha ubatizo ambapo aliwataka wazazi /walezi kuhakikisha watoto wote chini ya umri wa miaka mitano wanaoishi Manispaa Morogoro kuwa wamesajiliwa na kupata cheti cha kuzaliwa.

"Niwaombe wazazi/ walezi wapelekeni watoto wenu wakapate haki yao ya vyeti vya kuzaliwa, kwani zoezi hili la utoaji wa vyeti linafanyika katika ofisi zote za kata na vituo vyote vinavyotoa huduma ya baba, mama namtoto ( Kliniki), lakini pia cheti hiki cha kuzaliwa kinapatikana bila malipo huku ikibebwa na kauli mbiu ya " Mtoto anastahili cheti cha kuzaliwa , Mpe haki yake"Amesema Meya Kihanga

Pia ametoa wito kwa Madiwani pamoja wenyeviti wa mitaa wapite katika maeneo yao na endapo kuna watoto hawajasajiliwa waandikishwe.



*Wajumbe wa Kamati ya Mipango Miji na Mazingira Manispaa ya Morogoro wakiwa katika wakiwa katika ukaguzi w a Mradi wa ujenzi wa soko kuu la kisiasa*



*Wajumbe wa Baraza la Madiwani wakiwa katika kikao cha Baraza kuu wakiwa wamezingatia ukaaji wa mita 1 ili kujikinga na ugonjwa wa CORONA*

# MANISPAA MOROGORO YAZINDUA MAFUNZO YA MFUMO MPYA WA UHAMISHO WA WANAFUNZI KWA NJIA YA MTANDAO.



*Afisa Elimu Taaluma Manispa ya Morogoro , Jaribu Malambughi (aliyesimama) akifungua mafunzo kwa Walimu Wakuu wa Shule za Sekondari katika Ukumbi wa Mikutano wa Manispaa.*

Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kupitia Idara ya elimu Msingi na Sekondari wamezindua rasmi Mfumo mpya wa usajili na uhamishaji wanafunzi kwa njia ya mtandao.

Taarifa ya Mafunzo hayo imetolewa na Afisa Elimu Taaluma Manispaa ya Morogoro , Jaribu Malambughi katika Ukumbi wa Mikutano wa Manispaa Februari 19,2020 wakati wa uzinduzi wa mfumo huo .

Akizungumza na Waandishi wa habari, Malambughi, amesema kuwa faida za mfumo huo ni pamoja na kurahisisha kazi, kupata takwimu kwa haraka na kurahisisha mipango ya maendeleo shuleni pamoja na kujua hali ya mdondoko (utoro) kwa wanafunzi.

"Ndugu wakuu wa shule , walimu wa TEHAMA,taaluma mpo hapa kwa ajili ya kupata mafunzo juu ya mfumo mpya wa usajili na uhamishaji wanafunzi kwa njia ya mtandao, hivyo matumani yangu baada ya mafunzo haya kazi itafanyika vizuri na hatutegemei kupata malalamiko yoyote kuhusu mfumo huu wa kisasa ambao unalengo la kurahisisha kazi, kwahiyo tunajifunza kwa nadharia na vitendo ili tuelewe mfumo huu vizuri" Amesema Malambughi.

Aidha, mfumo huo unaojulikana kwa jina la Prems umetokana na maagizo ya barua ya Katibu Mkuu Wizara ya Elimu ya mwaka 2018 ambayo iliagiza wanafunzi wote walio katika shule binafsi na za Serikali

INAENDELEA UK... 16



***Afisa Utumishi Manispaa ya Morogoro, Waziri Kombo, akifungua Mkutano wa tathimini ya Ugonjwa CORONA kwa niaba ya Mkurugenzi wa Mnaispaa ya Morogoro, kwa Maafisa Afya na Watendaji wa Kata kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Manispaa, (kulia), Kaimu Afisa Afya Mkoa wa Morogoro, Prisca Gallet.***



***Afisa Mwandikishaji Jimbo la Morogoro Mjini , Sheilla Lukuba, akifungua semina ya Mafunzo kwa BVR Operators na Waandikishaji wasaidizi katika Ukumbi wa Mount. Uluguru.***

# WANANCHI WA MANISPAA YA MOROGORO WAMETAKIWA KUWA MSTARI WA MBELE KATIKA UCHANGIAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO.

INATOKA UK... 10

dombinu, afya na mengineyo ni jambo jema katika kuunga mkono juhudi za serikali zinazofanywa katika eneo lao.

RC Sanare , amesema katika miradi yoyote ya maendeleo jambo la kwanza linalotakiwa kufanyika ni kuona nguvu ya wananchi inatumika harafu Serikali wao wanamalizia.

Ametolea mfano wa Shule ya Msingi, Nanenane iliyopo Kata ya Tungi ina wanafunzi wapatao 2113 lakini changamoto iliyopo ni ukosefu wa madarasa 47 ambapo kwa sasa shule hiyo ina jumla ya madarasa 11 hivyo ili kufikia maendeleo ni lazima wananchi wachangie na Serikali kuona wapi wamekwama kwa vile miradi hiyo ni ya wananchi na siyo ya Serikali.

Amesema kwa mujibu wa sheria na taratibu kila darasa moja wanatakiwa kukaa wanafunzi wasiopungua 45.

Aidha amesema darasa moja kukusanya wanafunzi kupita kiasi ni sawa na mkutano wa wanafunzi na hata uelewa wao unakuwa ni mdogo ukilinganisha na darasa lenye watu wachache jambo ambalo linapelekea



*Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mhe. Loata Sanare akiwasili katika Viwanja vya Tubuyu Kata ya Tungi kwa ajili ya Mkutano na wananchi wa kata hiyo. (kushoto) Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe. Regina Chonjo*

kushuka kwa viwango vya elimu.

'Nitoe agizo kwa Afisa Utumishi, Afisa Tarafa pamoja na Watendaji wa Kata hii na wenye Viti wa Mitaa yote 12 katika Kata ya Tungi mkae chini muangalie ni kwa namna gani mnaweza kuweka mipango ili kuongeza madarasa yaliyopungufu na watoto wetu wakasoma vizuri na kufaulu,nafahamu hali ni mbaya tusiwalaumu tuu wananchi hawachangii lakini nyie viongozi lazima muonyeshe njia na mkazo na muwaambie ukweli wazazi kuwa wanapaswa kuchangia , tukifanya hivyo shule zetu zitapendeza na tutap-

INAENDELEA UK... 17

# WANAWAKE WAJASIRIAMALI IBUENI MIRADI YENYE TIJA NA INAYOTEKELEZEKA ILI MUWEZE KUREJESHA MIKOPO KWA WAKATI-RAS MOROGORO.

INATOKA UK... 10

amali wanapaswa kubadilika na kubuni biashara kubwa ambazo watakopeshwa vifaa badala ya fedha kwani Serikali ipo tayari kuwawezesha kununua vifaa na mashine za kuendeshea shughuli zao za uzalishaji.

Amesema Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Uongozi wa Rais Dkt. John Pombe Magufuli , imepitisha Sheria ya utoaji wa mikopo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu na kutengeneza kanuni za uendeshaji wa mfuko wa mkopo, ambapo sheria hiyo imeelekeza kila Halmashauri kutenga asilimia 10 ya mapato yake ya ndani ili kutoa mikopo isiyo na riba kwa makundi ya wanawake asilimia 4, vijana asilimia 4 na watu wenye ulemavu asilimia 2.

"Wanawake pamoja na wajasiriamali nawapongeza wote kwa juhudi za uzalishaji mali na mshikamano mnaouonesha katika kujenga Halmashauri yenu hususani katika suala zima la maendeleo, hii imepelekea kusonga mbele katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo inavutia na kuweza hata kwa Halmashauri nyingine kuja kujifunza kwenu hongereni sana, nimetoa hundi yenye



*Watumishi wa Manispaa Morogoro wakiingia uwanjani kwa maandamano wakati wa maadhimisho ya siku ya wanawake Duniani 08/3/2020*

INAENDELEA UK... 15

# HABARI PICHA KUONESHA MATUKIO MBALIMBALI





Muonekano wa kituo cha Afya Sina kilichopo kata ya Mafisa Manispaa ya Morogoro



Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Uchumi, Elimu na Afya Mhe. Spear Komanya (kushoto), Mwenyekiti wa Kamati ya Mipango Miji na Mazingira Mhe. Ally Kalungwana (kulia) wakiwa mbele ya Siwa katika kikao cha Baraza la Madiwani.



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa katika picha ya pamoja na viongozi wa Mkoa wa Morogoro alipozuru makaburi ya wahanga wa ajali ya moto katika makaburi ya kola  Machi 11, 2020



Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Sheilla Lukuba, akitoa pole kwa majeruhi wa Tembo, Edga Edbert (26) Mkazi wa Kata ya Tungi na John Mhaha (54) mkazi wa Kata ya Mkundi waliolazwa Hospitali ya Rufaa Morogoro



Muonekano wa sasa wa Ofisi ya Kata ya Uwanja wa Taifa baada ya kukamilika.

# WANAWAKE WAJASIRIAMALI IBUENI MIRADI YENYE TIJA NA INAYOTEKELEZEKA ILI MUWEZE KUREJESHA MIKOPO KWA WAKATI-RAS MOROGORO.

INATOKA UK... 13

thamani ya Shilingi Milioni 100,000,000 mnatakiwa fedha hizi kuzitumia kwa malengo mjitahidi kuwa waaminifu na kurejesha kwa wakati ili kutoa fursa kwa vikundi vingine ". Amesema Kalobelo.

"Kuna vikundi ambavyo vimefanya vizuri sana na vimerejesha mikopo kwa wakati na wanastahili pongezi, nami nichukue fursa hii kuwapongeza kwa kufanya kazi kwa bidii na kuzalisha lakini pia mmeonesha uaminifu katika matumizi ya fedha hizi za mkopo, ni dhahiri mmeweza kuongeza na kukuza mitaji yenu hata mkaweza kurejesha kwa wakati, wengine wote ambao bado mnadaiwa mjitahidi kurejesha ili kutoa fursa kwa wengine waweze kunufaika na mkopo huu, ni kuombe Mkurugenzi wa Manispaa uendelee kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani ili muwakopeshe wajasiriamali hawa wanaotafuta mitaji ya kukuza biashara zao " Ameongeza Kalobelo.

Amesema kuwa ili kuleta mapinduzi yaliyo ya kweli na ya kimaendeleo lazima uwekezaji ufanyike kwenye shughuli zinazoendana na uanzishwaji wa viwanda, kama sera ya nchi inavyoelekeza aliyoionyesha Mhe. Rais Dkt John Magufuli ya kauli mbiu ya hapa kazi tuu na kumuunga mkono kwa kutekeleza kwa vitendo ambapo katika awamu hii wanawake wamepewa nafasi kubwa kama nguvu kazi , wazalishaji na walezi wakubwa katika familia na kuwaomba wasimuangushe Mhe. Rais wafanye kazi kwa bidii na kuweka mikakati mizuri ya uzalishaji mali kwa kushirikiana na wanaume zao kuanzia ngazi ya familia na kusongesha Taifa mbele kiuchumi.

Aidha , amewataka wanawake waangalie maendeleo ya familia zao kwa ujumla katika nyanja zote kwani usawa au kutokuwa na usawa chimbuko lake linaanzia katika ngazi ya familia ambapo mfumo iyoyatarajia.

INAENDELEA UK... 22

# SALAMU ZA MSTAHIKI MEYA WA MANISPAA YA MOROGORO MHE.PASCAL KIHANGA.

INATOKA UK... 05

Sekondari tangu kuanza kwa mfumo wa Elimu ya Sekondari bila malipo Desemba, 2015 hadi kufikia Julai, 2019 Halmashauri ya Manispaa imepokea kiasi cha Tsh. 4,112,609,643.00 Kiasi hicho cha fedha kinajumuisha Ruzuku ya uendeshaji wa Shule, chakula kwa wanafunzi, posho ya madaraka kwa wakuu wa shule na fidia ya ada. Matokeo ya elimu bila malipo yameongeza uandikishaji kidato cha kwanza, mahudhurio na ufaulu wa wanafunzi.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016 hadi 2019, jumla ya fedha za Lipa Kulingana na Matokeo (EP4R) Tsh.556,408,570.00 zimepokelewa katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro. Fedha hizi zimetumika kwa ajili ya kurekebisha ikama ya walimu, ufuatiliaji na tathmini, ujenzi wa miundombinu ya madarasa, maabara na matundu ya vyoo.

Aidha Halmashauri imepokea Jumla ya Tsh. 1,534,201,480 zilizotolewa na Serikali ikiwa ni fidia kutokana na baadhi ya majengo na maeneo yanayomilikiwa na shule ya Sekondari Mji mpya iliyopata Tsh. 1,430,002,000.00 na shule ya sekondari Kingolwira iliyopata Tsh. 104,199,480.00 kutakiwa kupisha ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR).

Pia katika mpango wa Serikali wa uboreshaji wa shule kongwe, Manispaa ilipokea kiasi cha Tsh. 1,978,138,659.52 kwa ajili ya kuboresha shule ya sekondari Kilakala iliyopata Tsh. 935,584,126.72 na Shule ya Sekondari Morogoro iliyopata Tsh. 1,042,554,532.80.Ukarabati

umefanyika kwa kiwango cha hali ya juu hivyo kuboresha miundombinu ya elimu katika shule hizi.
Halmashauri imepokea Jumla ya Tsh. 300,000,000.00 zilizotolewa na Serikali ikiwa ni fedha kwa ajili ya umaliziaji wa maboma 24 katika shule 12 za sekondari katika Manispaa ya Morogoro hivyo kusaidia kupunguza tatizo la msongamano wa wanafunzi katika darasa moja. Wananchi wa Manispaa ya Morogoro wanashukuru sana kwa utatuzi wa changamoto mbalimbali zinazowakabili.
Vyumba vya madarasa katika shule za sekondari vimeongezeka kutoka 337 mwaka 2015 hadi kufikia vyumba 384 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 14. Ongezeko hili limepunguza msongamano darasani kwani uandikishaji wa wananfunzi pia umeongezeka.
Idadi ya matundu ya vyoo imeongezeka kutoka matundu 386 mwaka 2015 hadi kufikia matundu 541 mwaka 2019 katika shule mbalimbali za sekondari ikiwa ni ongezeko la asilimia 18.
Idadi ya vyumba vya maabara imeongezeka kwa asilimia 100 kutoka vyumba 10 mwaka 2015 hadi kufikia vyumba 20 mwaka 2019 maabara zote zipo katika hatua ya ukamilishaji.Manispaa imefanikiwa kuongeza asilimia ya uandikishaji wa wanafunzi wanaojiunga kidato cha tano

INAENDELEA UK... 21

# MANISPAA MOROGORO YAZINDUA MAFUNZO YA MFUMO MPYA WA UHAMISHO WA WANAFUNZI KWA NJIA YA MTANDAO.

INATOKA UK... 12

kuwa katika TSM9.
Pia mfumo huo utasaidia Maafisa elimu wa Manispaa kuweza kupandisha taarifa za wanafunzi kutoka shule, kupokea na kuidhinisha uhamisho wa wanafunzi pamoja na kuhariri taarifa zote za uhamisho.
Ili kuhakikisha mfumo huo unafanya kazi kikamilifu na kwa manufaa ya Elimu , utakuwa umegawanyika katika majukumu ya walimu Wakuu wa pande zote mbili ikiwemo wa Shule binafsi pamoja na Shule za Serikali.
Miongoni mwa kazi kwa upande wa Wakuu wa Shule za Serikali ni pamoja na kupokea na kuhakiki taarifa za wanafunzi kwa TSMS9 zao, kutuma, kupokea na kukubali maombi ya uhamisho pamoja na kusimamia usajili wa kidato cha kwanza kwa kuwapa namba ya usajili.
Pia kazi zitakazofanywa na Wakuu wa Shule binafsi (private) ni pamoja na kusajili wanafunzi katika mfumo, kuhamisha , kupokea na kukubali maombi ya uhamisho pamoja na kusimamia usajili wa wanafunzi kidato cha kwanza.
Aidha ,amesema kwa upande wa Wakuu wa shule binafsi mfumo huo utawasaidia kupakua templeti katika mfumo ambapo template hizo zitakuwa katika makundi ya umoja na wingi kwa ummoja itaruhusu kusajili mwanafunzi mmoja mmoja atakayefika baada ya wanafunzi wa pamoja kufanyiwa usajili.
Pia amesema katika usajili huo wa mfumo mpya , walimu wakuu hawaruhusiwi kusajili wanafunzi ambao hawajawasili shule kwa ajili ya masomo bali utasajili wale ambao wamewasili ndio watakao patiwa usajili ili kuepusha usumbufu kwa wazazi baada ya kubaini kwamba mwanafunzi amepelekwa shule binafsi itamlazimu mzazi aanze upya kufuatilia uhamisho.
Ameseisitiza suala la uhamisho ni lazima mzazi apewe Prem namba kutoka shule ambayo mwanafunzi anasoma ili kuweza kumruhusu kutafuta shule lakini prem namba hiyo katika mfumo wa uhamisho wa mtandao itadumu kwa muda wa siku 14 baada ya kupita kama mwanafunzi hajafanikiwa kupata shule itamlazimu mzazi kuanza upya maombi.



*Walimu wakuu shule za Serikali , Binafsi pamoja na walimu wa TEHAMA wakiendelea na mafunzo mfumo mpya wa uhamisho wa wanafunzo kwa mtandao leo.*

# WANANCHI WA MANISPAA YA MOROGORO WAMETAKIWA KUWA MSTARI WA MBELE KATIKA UCHANGIAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO.

INATOKA UK... 13

watoto tunataka shule zenye kutoa elimu bora"Amesema RC Sanare.

Pia Rc Sanare alitembelea ujenzi wa Zahanati ya Tungi na kuwataka watendaji kukaa na wananchi kufanya vikao na kuona jinsi ya kuweza kuchangia fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa jengo hilo ili liweze kutoa huduma kwa wananchi na kupunguza adha zinazowakumba kusafiri umbali mrefu kufuata huduma ya afya.

"Mna bahati sana wananchi wa hapa mmepata bahati ya kuletewa fedha za kutekeleza miradi hususani huu wa Zahanati ya kisasa lakini kasi ya wananchi katika kuchangia ni ndogo sana kwa ajili ya kuunga mkono jitihada za Serikali kumbukeni kuwa kwa kufanya hivyo ni kuvidhulumu vizazi vyenu viliyopo na vijavyo,taarifa niliyonayo ni kwamba wananchi wamechangia laki 7 tu , bado haitoshi ongezeni nguvu, Watendaji kaeni na watu wenu muwaeleze namna ya kuchangia hapa, isijetokea kiongozi akawarubuni na kuwaeleza msichangie, maendeleo hayana chama ,msiyumbishwe na wanasiasa wasio kuwa na wivu wa maendeleo " Amesisitizia RC Sanare.

Kwa upande wa Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe. Regina Chonjo, amesema katika maeneo yote aliyopita na kukagua yenye miradi ya ujenzi



*Mkuu wa Mkoa , Mhe. Loata Sanare, akisalimiana na mmoja wa Wananchi katika ziara ya kutembelea miradi ya Maendeleo Kata ya Tungi Manispaa ya Morogoro*

wa madarasa wananchi wanatakiwa kuchangia kwa kiasi kikubwa ili kuwatia moyo viongozi na kuendelea kuwapelekea miradi mengine.

"Kama wananchi mtashindwa kushiriki katika uchangiaji wa maendeleo katika ujenzi wa miradi inayowahusu , kiukweli jambo hilo litapelekea kuwavunja moyo viongozi kuendelea kuwapelekea miradi jambo ambalo litawaumiza wananchi, kikubwa kaeni katika vikao vyenu vya maendeleo mkishapitisha nileteeni ili tuone namna ya kuwapatia vibali vya michango ,mnatakiwa kuonesha angalau nguvu za wananchi kuliko kila kitu kuiachia Serikali wakati miradi ni ya kwenu wananchi" Amesema DC Chonjo.

Ameenda mbali zaidi na kuwataka wananchi kushiriki mikutano inayoitishwa na viongozi wao kuanzia ngazi za mitaa, ili wachangie mawazo yao katika masuala ya Maendeleo.

Hata hivyo, DC Chonjo, amewataka Watendaji wa Kata Manispaa ya Morogoro, kuwa chachu katika kuhamasisha shughuli za kimaendeleo na kuwa wavumilivu ili kuwapa nafasi viongozi walioko madarakani kutekeleza yale yaliyoelezwa katika Ilani ya Uchaguzi wa Chama Cha Mapinduzi CCM ya Mwaka 2015.

Naye Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Mhe. Pascal Kihanga, ameendelea kuwaeleza kuwa wanapochangia maendeleo na kuboresha miundombinu ndipo wanapoongeza pia kiwango cha ufaulu kwani wanafunzi wanakuwa na mazingira mazuri ya kujifunzia na walimu wanakuwa na mazingira mazuri ya kufundishia.

" Urithi pekee kwa watoto ni elimu hivyo ni jukumu la wazazi kuchangia sekta ya

elimu , elimu bila malipo haiondoi wajibu wako kama mzazi, haiondoi wajibu wako kama jamii hivyo ni lazima tuchangie shughuli za maendeleo ili kusaidia watoto wetu tusiachie Serikali kila kitu, Kila mmoja anawajibu wake, Kamati za shule zinawajibu wake na bodi za shule zina wajibu wake "Amesisitizia Meya Kihanga.
Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Mnaispaa ya Morogoro, Sheilla Lukuba, amewasihi wananchi wa Manispaa ya Morogoro hususani wa Kata ya Tungi kuwa na uchungu na maendeleo ya eneo lao na kuachana na migogoro isiyokuwa na tija kwani inawapotezea muda wa kufanya shughuli za maendeleo.
Mkazi wa Kata ya Tungi, Ayubu Mohamed, ameushukuru Uongozi wa Mkoa, Wilaya na Manispaa kwa ziara hizo huku akiamini ni moja ya njia ya kuwapelekea maendeleo na kuwataka Viongozi wasisite kufanya ziara kama hizo zenye malengo makubwa ya kutatua kero za wananchi wanyonge wenye matumani na Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi wa Mhe. Dkt John Pombe Magufuli.

# MANISPAA YA MOROGORO YAUNGANA NA TASWO KUWAFARIJI NDUGU WA MAREHEMU WA AJALI YA MOTO MSAMVU.

INATOKA UK... 08

wajane wakiwa na watoto hali hii imefanya familia zao ziwe tegemezi kwa kiasi fulani, hivyo niseme kuwa upo uhusiano wa moja kwa moja kati ya ukuaji wa uchumi wa nchi na utengamano wa kijamii kwa wananchi wa nchi husika, kamwe hatuwezi kutenganisha maendeleo ya kiuchumi ,kisiasa, kitamaduni na Ustawi kwa jamii katika nchi kwani yote haya hutegemeana , na tukumbuke kwamba mahali ambapo ustawi wa kweli wa Jamii haupo hata maendeleo ya kweli katika nyanja zote huathirika na wakati mwingine kutokuwepo kabisa, hivyo TASWO mmetushika mkono kilichobakia Ustawi wa Jamii Manispaa pamoja na viongozi wa Kata hii msisubirie mwaka kwa mwaka mjenge utaratibu wa kuwatembelea hawa ndugu zetu na kuwasaidia kile mlichonacho hata kama sio pesa hata ushauri wa nini wafanyaje itakuwa jambo la faraja sana kwao na kujisikia wanathaminiwa ”Amesema Mhe. Kihanga.
Pia , amesema Serikali imewatambua marehemu hao hadi kufikia kuwatengenezea uzio katika eneo la makaburi na mpango uliopo kwa sasa ni kuwajengea makaburi ya pamoja yenye kufanana na kuweka mnara mkubwa utakao kuwa na majina yao marehemu



Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Mhe. Pascal Kihanga , akikabidhi daftari kwa ndugu wa marehemu, (kulia), Diwani wa Kata ya Mwembesongo, Mhe. Ally Kalungwana.

wote ili iwe sehemu moja ya kuwakumbuka na ndugu wakiwa wanataka kuwaona itakuwepo sehemu kwa ajili ya dua kwa dini zote.
Amesisitiza huku akisema kuwa ndugu wa marehemu wajenge utamaduni wa kuwaombea ndugu zao mara kwa mara na sio kusubiria kila mwaka kama Serikali ilivyojiwekea utaratibu wa kuwakumbuka.
Katika hatua nyingine, amesema maendeleo ya Ustawi wa Jamii ni muhimu sana kama ilivyo maendeleo katika Uchumi na hasa kwa sasa ambapo Taifa linafanya kila jitihada ya kufikia malengo ya kuwa na uchumi wa kati na Viwanda ifikapo mwaka 2025, ambapo hayo yote yanaenda sambamba na kuhakikisha uhusiano wa Watu na Ustawi wa Jamii kwa ujumla upo katika hali ya kuridhisha .
Naye Mwenyekiti wa TWASO Taifa, Dr. Mariana Makuu, amesema katika kuunga mkono juhudi zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano Chini ya Rais , Mhe. Dkt. John Magufuli , kwa kutambua umuhimu wa maadhimisho hayo wameona ni vyema wakawakumbuka wajane pamoja na tegemezi wa Marehemu waliofariki kwa ajali

INAENDELEA UK... 20

# MANISPAA YA MOROGORO YANUNUA PIKIPIKI 7 ZENYE THAMANI YA SHILINGI MILIONI 23 KWA AJILI YA KATA ZA PEMBEZONI.

Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro imenunua Pikipiki saba (7) aina ya YAMAHA zenye thamani ya Shilingi Milioni 23,100,000/= pamoja na kodi (VAT) kupitia fedha za Mradi wa uboreshaji Miji (ULGSP) katika bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020 kwa ajili ya kuwajengea uwezo watumishi kwa kuboresha utendaji kazi wao.



*Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Mhe. Pascal Kihanga, akiwasha Pikipiki katika hafla fupi ya makabidhiano ya Pikipiki hizo kwa Kata zilizopo Pembezoni mwa Manispaa ya Morogoro.*

Akizungumza na Waandishi wa Habari mara baada ya makabidhiano hayo ya Pikipiki ,Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Mhe. Pascal Kihanga, amesema Pikipiki hizo zimenunuliwa mahsusi kwa ajili ya Kata za Pembezoni ambapo pikipiki nne (4) wamepatiwa Kata ya Luhungo, Mzinga , Mkundi pamoja na Kingolwira.

Amesema Pikipiki tatu (3) zimebakia Ofisi Kuu ya Manispaa ya Morogoro kwa ajili ya kuimarisha utendaji kazi wa Halmashauri.

"Tunaipongeza sana Manispaa kwa kuwa na jicho la tatu kununua Pikipiki hizi, Kata hizi za pembezoni zinachangamoto sana haswa kwa Watendaji wake wanashindwa kuwafikia Wananchi kwa urahisi na kushindwa kutoa huduma lakini kwa hiki walichokifanya kitatoa mwanya mzuri wa Watendaji kuwahudumia wananchi wao ipasavyo, lakini niwaombe na kumuomba Mkurugenzi wetu wa Mansipaa kwamba Pikipiki hizi zitumike katika muda wa kazi baada ya hapo wewe mtendaji endelea na mambo yako mengine weka chombo hicho nyumbani kwani isijekuwa Manispaa imefikiria kuleta maendeleo harafu maendeleeo hayo yakageuka vifo tunajuana tabia zetu sasa tuvilinde na kuvithamini"Amesema Mhe. Kihanga.

Hata hivyo amewataka Watendaji wa Kata hizo, kuvitumia vyombo hivyo vya Moto kwa malengo yaliyokusudiwa na sio kuvitumia kwa ajili ya kugeuza kuwa Bodaboda na kujipatia kipato kwa atakaye kiuka utaratibu atachukuliwa hatua za Kisheria .

Katika hatua nyingine, amewapongeza wataalamu wa Manispaa na kuwaomba mara baada ya Miradi iliyopo kukamilika waanze kufikiria miradi mipya kwani anaamini Bajeti ijayo ya Mwaka wa fedha wa 2021/2022 Manispaa itakuwa na fedha za kutosha na kuweza kuwa na bajeti kubwa ya kihistoria.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Sheilla Lukuba, amesema Manispaa imetoa Pikipiki hizo kwa ajili ya kurahisisha huduma kwa Wananchi na kuhakikisha huduma bora zinapatikana katika Kata hizo.

Amesema kuwa matarajio yake ni kuona kuwa Pikipiki hizo zinarahisisha kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali kwani hata maeneo yasiyofikika kwa urahisi kwa gari sasa yatafikika.

"Tuvitunze vyombo hivi, Serikali yetu ya Awamu ya Tano chini ya Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli, imeonyesha moyo wa kuthamini kazi zetu nasi tuvipe heshima na kuvitumia kwa malengo tarajiwa, tusiende kuvigeuza bodaboda na tutaweka utaratibu yule ambaye ataki-

uka utaratibu huu tutamchukulia hatua kali za kisheria niwaombe Watendaji chapeni kazi tuendelee kuwahudumia Wananchi wetu katika Utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi CCM katika kufikia adhima ya Tanzania ya Viwanda na Uchumi wa Kati"Amesema Sheilla.

Aidha, Mkurugenzi amewataka Watumishi wote wa Manispaa kufanya kazi kwa bidii ili kuweza kufikia malengo na kutoa huduma bora kwa Wananchi.



*Afisa Utumishi wa Manispaa ya Morogoro , Waziri Kombo, (kushoto), akisoma taarifa fupi ya Manunuzi ya Pikipiki kwa ajili ya Kata zilizopo pembezoni wa Manispaa ya Morogoro, (kulia), Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Sheilla Lukuba, (katikati), Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Mhe. Pascal Kihanga.*

# MANISPAA YA MOROGORO YAUNGANA NA TASWO KUWAFARIJI NDUGU WA MAREHEMU WA AJALI YA MOTO MSAMVU.

INATOKA UK... 18

ya Moto Msamvu baada ya Lori la Mafuta kushika moto.
Amesema tukio hilo litabakia kuwa la kihistoria hivyo wao ona ni vyema wakawakumbuka kwa kuwapatia vyakula , madaftari, peni , sabuni pamoja na mafuta ya kula ili waendelee kujikimu kimaisha katika kipindi kigumu wanachopitia.

Dr. Makuu amesema wataalamu wa ustawi wa jamii wameendelea kubaki kama kichochoeo cha kuimarisha mahusiano ya watu wote na hili wanalifanya katika maisha yao ya kila siku ya kitaaluma na kazi na pale inapotokea mahusiano ya watu yana shaka au dosari basi kazi kubwa ya kufanya ni ya kurejesha mahusiano .

"Kila Mtanzania popote alipo anayo haki ya kupata huduma bora za Ustawi wa Jamii na kulinda utu na heshima yake, heshima ya mtu mwingine ikiwa ni pamoja na heshima ya Taifa kwa ujumla, ambapo ndio maana hata Ilani ya Chama Tawala kinachoongoza Serikali yetu imeangalia kwa kina masuala ya Ustawi wa Jamii katika Ibara zake tofauti" Amesema Dr. Makuu.

Amesema kuwa katika kuadhimisha Sikukuu hiyo ya Kitaifa, TASWO Morogoro imeona umuhimu wa kukuza mahusiano ya watoa huduma za Ustawi wa Jamii na wapokea huduma kwa kuzitegemeza baadhi ya familia ambazo ziliwapoteza ndugu wa karibu katika janga la mlipuko wa gari la mafuta ya Petroli lililotokea tarehe 10 Agosti 2019.

Amesema TASWO inatanguliza shukrani kwa NMB Benki,na CBO na wote walioonyesha utayari wa kuwaunga mkono katika maadhimisho ya Siku ya Ustawi wa Jamii Duniani (WORDL SOCIAL WORK DAY) iliyoadhimishwa Kitaifa Manispaa ya Morogoro ambapo maadhimisho hayo hufanyika duniani kote kila mwaka kuanzia wiki ya pili mpaka ya mwisho wa mwezi wa tatu ambapo kauli mbiu inasema 'UMUHIMU WA KUKUZA MAHUSIANO YA WATU HASA KATIKA KULETA MABADILIKO".

Kwa upande wa Afisa Ustawi wa Jamii Manispaa ya Morogoro, Bi. Sidina Mathias, akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, amekishukuru Chama cha TASWO kwa moyo waliouonyesha kwani zipo sehemu nyingi zenye shida lakini wameona Manispaa ya Morogoro kuwa sehemu moja wapo ya kufanikisha siku hiyo ya Maadhimisho ya Siku ya Ustawi wa Jamii Duniani.

"Nawapongeza sana ndugu zetu wa TASWO ,hiki walichokionyesha kimetufariji sana , tunaomba ushirikiano huu wa kitaaluma uendelee ili kuleta mafanikio chanya katika nyanja mbalimbali hususani katika kuwasaidia watu ambao wamekosa faraja na tegemezi katika familia, sisi kama Manispaa tunaungana kwa pamoja na hili lisiishie hapa hata katika maadhimisho mengine tuendelee kuwakumbuka watu wenye



*Diwani wa Kata ya Mwembesongo, Mhe. Ally Kalungwana, akizungumza na Ndugu wa marehemu waliojitokeza katika maadhimisho ya Siku ya Ustawi wa Jamii Duniani yaliyofanyika Kitaifa Manispaa ya Morogoro, Kata ya Mwembesongo.*

changamoto katika jamii na hata vile vituo vya kulelea Wazee na watu wanaoishi katika Mazingira magumu na yatima" Amesema Sidina.
Diwani wa Kata ya Mwembe-songo, Mhe. Ally Kalungwana, ameushukuru Uongozi wa TASWO kwa faraja walioinye-sha wakishirikiana na Manispaa ya Morogoro kwani kitendo hicho kitaamsha hali ya ndugu wa marehemu kujiamini na kuona wana thamani sawa na watu wengine.
Aidha amewaonya wananchi wa Manispaa ya Morogoro hususani wakazi wa Kata yake kuacha tabia ya kukimbilia vitu vyenye madhara wanapoona kuna dalili hizo au kuna matukio yenye madhara yame-tokea kwani huatarisha maisha yao.




*Mwenyekiti wa TASWO Taifa, Dr. Mariana Makuu, akizungumza na Ndugu wa Marehemu katika siku ya Maadhimisho ya Siku ya Ustawi wa Jamii Duniani, (kushoto) Afisa Ustawi wa Jamii Manispaa ya Morogoro, Sidina Mathias, Meya Manispaa ya Morogoro, mhe. Pascal Kihanga, (kulia), Diwani wa Kata ya Mwembesongo , Mhe. Ally Kalungwana.*

# SALAMU ZA MSTAHIKI MEYA WA MANISPAA YA MOROGORO MHE.PASCAL KIHANGA.

INATOKA UK... 16

kutoka 95 mwaka 2015 hadi 107.5 mwaka 2019 ikiwa ni matokeo ya sera ya elimu bila malipo iliyoanza kutekelezwa mwaka 2015.
Kidato cha sita ufaulu ume-ongezeka kutoka asilimia 99.6 kwa mwaka 2015 hadi 99.8 mwaka 2019. Aidha Hal-mashauri imefanikiwa kununua jumla ya pikipiki 29 kwa ajili ya waratibu elimu Kata iliku-waboreshea mazingira ya kazi hasa kufanya ufuatiliaji na usimamizi wa uendeshaji wa shule katika maeneo yao.
Aidha majengo ya utawala yameongezeka kutoka 5 mwaka 2015 hadi kufikia majengo 8 mwaka 2019 katika kata mbalimbali na tumefanikiwa kukamilisha ujenzi wa Ofisi ya kisasa ya Kata ya Mji Mkuu yenye mahitaji muhimu ikiwe-mo ukumbi wa mikutano, huduma ya choo, nk. Kukami-lika kwa Ofisi hii kumewezesha kuongeza ufanisi wa utoaji huduma kwa wananchi.Aidha Majengo mbalimbali ya ofisi za kata yapo katika hatua za umal-iziaji ikiwepo kata ya Uwanja wa Taifa,Kingolwira,Kiwanja cha Ndege nk.
Kwa upande wa sekta ya Afya Halmashauri inaendelea na utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa kuhakiki-sha mapato yanaongezeka. Kabla ya mwaka 2015 mapato yalikuwa Tsh. 294,392,885.61 sawa na asilimia hamsini (50%) ukilin-ganisha na kipindi cha awamu ya tano ambapo mapato yameongeze-ka hadi kufikia Tsh.440,774,761 sawa na asilimia 83.Ongezeko la mapato haya ni kutokana na utumiaji wa mfumo wa GOT HOMIS katika vituo na usimamizi mzuri wa uendeshaji wa huduma za Afya.
Awali huduma za kujifungua zilipatikana katika vituo vitatu (3) tu.Katika kipindi cha awamu ya tano huduma za kujifungua zimeongezeka na kufikia vituo 7.Aidha Hal-mashauri imekamilisha ujenzi wa wodi ya wazazi katika kituo cha afya Sabasaba chenye thamani ya Tsh. 129,923,850. Ujenzi wa wodi hiyo umepun-guza msongamano mkubwa wa kina mama wajawazito katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa (MRRH) kwani kwa sasa wastani wa wajawazito70 hujif-ungulia kituoni hapo kwa kila mwezi ukilinganisha na mwaka 2015 ambapo kituo hicho kili-kuwa hakizalishi kabisa.
Vitanda vyenye thamani ya Tshs 13,550,000 vimenunuliwa kwa ajili ya kuanzisha huduma hiyo. Awali Halmashauri haiku-wa na mashine zozote za Ultra sound katika vituo vya kutolea huduma. Katika kipindi cha awamu ya tano Halmashauri imefanikiwa kununua mashine za Ultra-sound mbili (2) zenye thamani ya Tsh. 90,000,000 katika kituo cha Afya cha Mafiga na Kingolwira.
Ununuaji wa mashine hizo umeboresha upatikanaji wa huduma za ultra sound katika vituo vya kutolea huduma tofauti na kabla ya hapo ambapo wateja hasa wajawazito walilazimika kuipata huduma hiyo hospitali ya mkoa tu.
Kipindi cha nyuma kituo kiliku-wa kinatoa huduma za kinywa

INAENDELEA UK... 24

# WANAWAKE WAJASIRIAMALI IBUENI MIRADI YENYE TIJA NA INAYOTEKELEZEKA ILI MUWEZE KUREJESHA MIKOPO KWA WAKATI-RAS MOROGORO.

INATOKA UK... 15

Pia amechukua fursa ya kuwakumbusha wakina mama waendelee kukemea vitendo vay ukatilia wa kijinsia vinavyoendelea katika jamii,na amesisitiza ushirikiano wa kamati za kupinga na kutokomeza ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto katika ngazi za mitaa, Kata hadi Manispaa kushirikiana na Jeshi la Polisi Dawati la Jinsia katika kutoa elimu ya masuala ya ukatili na kutoa taarifa za matukio ya ukatili yanayofanyika katika maeneo yakiwemo ubakaji na ulawiti ili hatua za kisheria zichukuliwe kwa wanaotenda makosa hayo.

Ametoa wito kwa wanawake na kuwaeleza kuwa Serikali chini ya Rais Dkt. John Magufuli, imeanzisha programu mbalimbali ikiwamo programu ya Elimu bure, Bima ya Afya iliyoboreshwa (CHF), na mkakati wa utoaji wa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano na kuagiza idara zote zinazohusika na programu hizo kuhakikisha wanasismamia huduma hizo ipasavyo  na kuwaasa  wanawake kupitia mikutano yao ya vikundi vya kijamii kama vile VICOBA, SACCOS wapeane taarifa za kimaendeleo na wawe tayari kuhudhuria  mikutano ya Mitaa inayoandaliwa kwa mujibu wa sheria kwani huko ndiko chimbuko la taarifa za kimaendleeo na fursa mbalimbali zinazojitokeza.

Hata hivyo amewataka wakina mama wajitokeze kwa wingi katika kipindi cha uchaguzi mkuu Oktoba 2020 ili waweze kugombea nafasi za uongozi katika maeneo yao jambo ambalo litadhihirisha kwamba wanatekeleza kwa vitendo kauli mbiu ya “KIZAZI CHA USAWA KWA MAENDELEO YA TANZANIA YA SASA NA YA BAADAYE” huku akiwapongeza wanawake wote waliojitokeza katika kugombea nafasi uchaguzi wa Serikali za Mitaa na waliojitokeza katika kujiandikisha kwenye daftari la kudumu la wapiga kura.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa manispaa ya Morogoro, Sheilla Lukuba, amesema Manispaa ya Morogoro inatambua na kuthamini juhudi zinazofanywa na wajasiriamali wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu ambapo katika kipindi cha fedha mwaka 2019/2020 manispaa imetoa kiasi cha shilingi milioni 100 kwa ajili ya mikopo ambapo kati ya hizo shilingi milioni 45,5000,000.00/= zimetolewa

INAENDELEA UK... 27



*Waziri wa OR-TAMISEMI Selemani Jafo akijiandaa kukata utepe kama ishara ya uzinduzi wa shule ya Sekondari ya Mji Mpya. wa pili kutoka kulia (mwenye suti nyeusi) ni Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro Mhandisi Emannuel Kalobelo*




*Afisa Mwandikishaji Jimbo la Morogoro Mjini, Sheilla Lukuba, akiwa na Afisa Mwandikishaji Msaidizi wa Jimbo la Morogoro Mjini, Waziri Kombo katika kuangalia zoezi la uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura katika kituo cha Kata ya Kihonda.*

# DC CHONJO ASHUSHA MAELEKZO NA KUWATAKA WAMILIKI WA HOTELI KUWA WAKALI KATIKA KUWAPOKEA RAIA WA KIGENI

MKUU wa Wilaya ya Morogoro, Mhe. Regina Chonjo, amekutana na Wamiliki pamoja na Meneja wa Hoteli Wilayani Morogoro kwa ajili ya kuwapatia elimu pamoja na maelekezo kutoka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Magufuli, juu ya kuwapokea raia wa kigeni katika Hoteli zao ikiwa na lengo la kujikinga na Ugonjwa wa CORONA.

Mkutano huo umefanyika Aprili 3, 2020 katika Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.



*Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe. Regina Chonjo , akizungumza na Wamiliki pamoja na Mameneja wa Hoteli kwa ajili ya kutoa maelekezo juu ya kujikinga na Ugonjwa wa CORONA, (kushoto), Katibu Tawala Wilaya ya Morogoro, Ruth John, (kulia) Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Sheilla Lukuba*

Akizungumza na Wamiliki hao na Mameneja wa Hoteli , amesema lengo la mkutano huo ni kuwapa maelekezo yaliyotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Magufuli juu ya kuwapokea raia wa kigeni

INAENDELEA UK... 25

# WAZIRI JAFFO ARIDHISHWA NA KAZI ZA TARURA MANISPAA YA MOROGORO.

INATOKA UK... 03

ka viraka, kwa hiyo ni mategemeo yangu barabara hii iwe na uhakika wa miaka 20 na wakandarasi tunaowapa kazi za ujenzi wa barabara wasiwe wababaishaji, na nawaagiza TARURA muwabane wakandarasi watutengenezee barabara zenye ubora lakini wahakikishe kwamba mifereji yote na kalavat nazo mzijenge kama mlivyojenga katika barabara hii kwani hii mifereji ingekuwa dhaifu tungeshuhudia uharibifu mkubwa hapa, niwapongeze kwa kazi nzuri hamjawahi kuniangusha Manispaa ya Morogoro mnafanya kazi kwa maelekezo hongereni sana ”Amesema Jaffo.

Katika ziara yake hiyo, Mhe.-Jaffo amewaagiza Meneja wa TARURA wote nchi nzima kuanzia wa Mikoani hadi Halmashauri kuhakikisha wanapita mara kwa mara madaraja na kuyakagua ikiwamo kusafisha mifereji inayozibwa kwa mrundikano wa mchanga na matope ili wakati wa mvua isilete madhara kwa wananchi na kuharibu miundombinu.

Kwa upande wa Meneja wa TARURA Manispaa ya Morogoro, Mhandisi James Mnene, amemshukuru Waziri Jaffo kwa pongezi na tamko lake la kutaka fedha zote za matengenezo ya kila siku za Barabara zitumike katika kuboresha miundombinu ya mifereji , kalavati pamoja na madaraja ili kuepusha madhara ya uharibifu wa miundombinu na madhahara kwa wananchi hususani katika kipindi cha Mvua.

Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI Mh. Selemani Jaffo, alihitimisha ziara yake kwa kwa kukagua ujenzi wa Shule ya Sekondari Morogoro baada ya kutembelea mradi wa Soko kuu la Kisasa linaloendela na Ujenzi katika Manispaa ya Morogoro katika Kata ya Mji Mkuu.

# SALAMU ZA MSTAHIKI MEYA WA MANISPAA YA MOROGORO MHE.PASCAL KIHANGA.

INATOKA UK... 21

na meno ambazo hazikutumia vifaa vya kisasa yaani (Digital). Katika kipindi cha awamu ya tano Idara ya Afya inakamilisha mchakato wa kuboresha huduma za meno katika kituo cha Afya sabasaba na kuzifanya za kisasa ambapo mashine ya meno (complete dental chair) na mashine ya x-ray ya meno (Digital) zenye thamani ya shilingi 38,000,000 zimefanyiwa taratibu za manunuzi na zitaanza kutumika hivi karibuni. Aidha ukarabati wa jengo la kitengo hicho utafanyika kwa gharama za Tsh. 10,000,000 ili kuweka miundombinu mizuri ya utoaji wa huduma za meno. Pia kwa sasa Halmashauri imeongeza mashine ya full-blood picture 1 (mpya) yenye thamani ya Tshs. 7,000,000 katika kituo cha Afya Uhuru ambayo hupima vipimo mbalimbali pamoja na mashine ya full blood picture mbili (2) katika kituo cha Afya Saba saba na Kingolwira pia vipimo mbali mbali vimeongezeka kama vipimo vya Homa ya ini na typhoid fever. Hali ya upatikanaji wa dawa katika vituo vya kutolea huduma imeendelea kuimarika kulingana na taarifa za Mfumo wa upatikanaji dawa muhimu. Aidha, vyanzo vikuu vya ununuzi wa dawa ni fedha zinazotolewa na serikali kuu kupitia mfumo wa ILS, Mfuko wa pamoja (HBSF) na fedha za uchangiaji huduma (Cost Sharing).

Natumia fursa hii kuipongeza Serikali ya awamu ya tano kwa kuongeza bajeti ya dawa kutoka asilimia 80% hadi 94% kwa mwaka 2019.

Halmashauri kwa kushirikiana na wafadhili wa wazee (MOROPEO) wamepokea mikoba yenye vifaa vya matibabu kama BP mashine vyenye thamani ya Tshs. 14,000,000. Pia Manispaa ina jumla ya wazee 15,631 na mpaka sasa imetoa vitambulisho kwa wazee 4002. Aidha, katika kutekeleza utaratibu wa matibabu kwa wazee, madirisha ya matibabu kwa wazee yamefunguliwa na yanafanya kazi katika vituo vyote vinne vya Afya vya umma. Katika zahanati ambazo idadi ya wateja si wengi na kuna ufinyu wa miundombinu matangazo ya mpishe "MZEE AHUDUMIWE KWANZA" yanatekelezwa kwa vitendo na wazee wanapewa kipaumbele. Wananchi wa Manispaa ya Morogoro wanaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuboresha miundombunu ya Afya katika Manispaa yetu kwani Afya ndio uhai wa wananchi.

Sekta ya Mipango Miji, Ardhi na Maliasili inaendelea kusimamia rasilimali ardhi kwa manufaa ya wananchi. Hadi sasa Halmashauri ya Manispaa Morogoro imefanikiwa kuandaa Mpango kabambe (Master Plan) katika Mitaa 294 ya kata 29 ambayo iko katika hatua ya nane na ya mwisho kabla ya kuidhinishwa.Kuanzia 2015-juni 2019 jumla ya hati miliki

INAENDELEA UK... 28



*Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Sheilla Lukuba (kushoto), Katibu Tawala Wilaya ya Morogoro Mjini ,(wapili kushoto), Meya wa Manispaa ya Morogoro, Mhe. Pascal Kihanga (wanne kulia), wakiwa katika kikao cha Kamati ya Ushauri Wilaya kupitia mapendekezo ya bajeti ya Manispaa ya Morogoro ya mwaka 2020/2021*



*Waziri wa OR-TAMISEMI Selemani Jaffo akiwa katika picha ya kumbukumbu na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Morogoro*



*Wajumbe wa kamati ya Fedha na Uongozi wakiwa katika ukaguzi wa Mradi wa ujenzi wa stendi ya Daladala Mafiga*



*Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe. Regina Chonjo (kulia)akimkabidhi Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mji Mkuu, mifuko 50 ya Saruji kwa ajili ya ukarabati vwa shule hiyo*

# DC CHONJO ASHUSHA MAELEKZO NA KUWATAKA WAMILIKI WA HOTELI KUWA WAKALI KATIKA KUWAPOKEA RAIA WA KIGENI

INATOKA UK... 23

katika Hoteli zao ikiwa na lengo la kujikinga na Ugonjwa wa CORONA.

Amesema kumekuwa na utaratibu wa kuwakumbatia watu wasio julikana katika nyumba za kulala Wageni hususani katika Hoteli jambo ambalo ni baya sana hasa katika kipindi hiki cha kupambana na vita dhidi ya Ugonjwa wa CORONA.

Chonjo, amesema ni wakati wa kushirikiana na kuwa kitu kimoja kati ya Serikali na Wamiliki wa Hoteli kwa ajili ya kuwachunga na kuwatolea maelezo raia na washukiwa wanaoingia katika Hoteli zao kwa kuwawekea ulinzi endapo watawabaini ili kutoeneza ugonjwa huo.

"Tumeitana hapa kwa lengo moja, Mhe. Rais Dkt John Magufuli ameshatoa maelekezo kwa Hoteli zote jinsi ya kuweka umakini na wageni wanaotoka nchi zilizo na historia ya Ugonjwa huo, kwahiyo tunatakiwa tushirikiane kwa pamoja na tutoe ushirikiano wa kuweka mazingira kwa washukiwa hao, kama utaona mtu haeleweki toa taarifa au ameingia katika Hoteli yako ni raia wa kigeni muhifadhi katika chumba chenye huduma zote ndani kwa muda wa siku 14 na asitoke nje baada ya hapo piga simu kwa wataalamu wa afya watakuja kumuangalia kitaalamu na baada ya siku 14 kama zitaonekana dalili za Ugonjwa huo atachukuliwa na Wataalamu kufikishwa katika Karantini zetu tulizozitenga maeneo, hawa sio kwaml a wana ugonjwa ila tahadhar ni muhimu na chumba chake h ıkikisheni muhudumu hair gii ndani , wala ndugu pamoja n ı familia zao na huduma za chak ıla anatakiwa awekewe nje ya mlango na kumgongea ili k ıkifuata na upande wa ngu zao lazima zifuliwe kwa da va na kuwekwa katika vikapu zi ikauka zipelekwe mlangoni kama ilivyo huduma nyengi e , lakini baada ya mtu huyo kumaliza karantini hapo Hotelini chumba chake kitatakiwa kufanyiwa Farmigation ya hali ya juu na huyo mtu atajaza fomu ya kuonyesha kwamba alikuwa Karantini na yupo tayari kuwepo uraiani" Amesema DC Chonjo.

Aidha, amewatahadharisha Wamiliki kuacha tama ya pesa badala yake wawe makini katika kutanguliza afya za wahudumu wao pamoja na za Wananchi kwa ujumla kwani wanaweza kuwa na tamaa ya kupokea fedha nyingi wakati huo wanaleta ugonjwa na kuhatarisha maisha ya watu wengine.

Pia amesema ni vyema kujenga ushirikiano mzuri baina ya Wamiliki wa Hoteli, Maafisa Uhamiaji pamoja na Wataalamu wa afya ili wanapombaini mtu haeleweki au ana dalili za ugonjwa huo wakatoa taarifa mapema sana ili hatua za kitaalamu ziweze kuchukuliwa.

Hata hivyo,amewataka Wamiliki wa Hoteli wote kuanzia tarehe 6, Aprili siku ya Jumata-

tu , kila mmiliki awe ametoa taarifa ya huduma za bei katika vyumba vya kulala kwa Hoteli nzima na kukabidhi timu ya Wataalamu watakao pita mitaani kukusanya taarifa hizo ili wale wanaotaka kwenda kupata huduma kama itatokea anawekwa mtu Karantini basi alipe kulingana na uwezo wake wa fedha katika upatikanaji wa huduma hizo ili isije kuleta shida kwa wamilki wa Hoteli baada ya kushindwa kulipa huduma .

Amesema kuwa baada ya ugoinjwa huo kuingia hapa nchini, Wilaya ya Morogoro iliunda Kamati za Karantini, hivyo ni jukumu sasa la Kamati hiyo kuanza kufuatilia bei za vyumba vyote kwa kila Hoteli ili kuweza kuona jinsi ya kuwasaidia Wageni wanaotaka Hoteli kwa bei tofauti tofauti kulingana na uwezo wake wa kifedha.

Katika kuhitimisha mkutano huo, amesema kama watu wote watamuomba Mwenyezi Mungu na kuzingatia maelekezo ya Wataalamu pamoja na Viongozi wa Ngazi za juu na kufuata maelekezo yote basi ugonjwa huo kwa Wilaya ya Morogoro hautafika .

Katika hatua nyengine, DC Chonjo, aliwataka Waganga wakuu wa Manispaa ya Morogoro pamoja na Morogoro Vijini kuwasilisha taarifa ya jinsi walivyochukua hatua za kupambana na Ugonjwa wa CORONA.

Kwa upande wa Mganga Mkuu wa Morogoro Vijijini, Dr. Robert Manyenyere , amesema wao walitumia njia za kutoa elimu katika maeneo yote yenye mikusanyiko ya watu , kutenga eneo la Karantini katika Kituo cha afya cha Ngerengere, kutenga eneo la Karantini katika Bwawa la Mwalimu Nyerere, pamoja na kuweka kituo cha Karantini katika Mradi wa Mwendokasi kwani eneo hilo limekuwa na wageni wanaoendelea na ujenzi huo.

Naye Kaimu Mganga Mkuu wa Manispaa ya Morogoro, Dr. Gosbert Kalunde, amesema Manispaa ya Morogoro imetoa elimu katika meneo yote yenye mkusanyiko ikiwamo Nyumba za wageni, mama ntilie ,Matangazo katika Vyombo vya Habari, vituo vya Bajaji, Bodaboda, Madukani, Stendi za Daladala pamoja na Stendi kubwa ya Mabasi yaendayo Mikoani ya Msamvu lengo likiwa kuwaelimisha wananchi jinsi ya kujikinga na Ugonjwa wa CORONA.

Amesema tayari Manispaa ilishaanda timu ya Wataalamu wa Karantini na eneo ilishatenga lililopo katika Ujenzi wa Hospitali ya Manispaa iliyopo Kata ya Mkundi ambapo washukiwa wote wa Ugoinjwa wa CORONA wanapekwa huko kwa jili ya vipimo vya awali.

Pia amesema wamenunua vifaa tiba kwa kuwakabidhi wauguzi waliopo katika Vituo vya afya pamoja na wale waliopo katika Karantini hiyo kuvitumia endapo watapata mshukiwa wa ugonjwa huo.

Licha ya jitihada hizo, lakini amesema wapo viongozi wa Manispaa kwa fedha zao wenyewe waliamua kuiunga Mkono Serikali kwa kugawa ndoo za maji , sabuni pamoja na vitakasa mikono kwa jili ya kuwakinga wananchi wao na ugonjwa huo.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Sheilla Lukuba, amesema baada ya agizo la Waziri Mkuu, Mh Kassim Majaliwa la kuwataka wafanyabiashara kuuza vifaa tiba kwa bei elekezi, yeye pamoja na timu yake ya Wataalamu walitembelea maduka hayo na kupiga faini baadhi ya maduka kwa kukiuka agizo la Waziri na kutoza faini kwa upande wa magari ambayo yalikiuka pia maagizo ya kuwawekea maji sabuni na vitakasa mikono abaria wao.

Paul Haule ambaye ni Mmiliki wa Bambo Guest House, ampongeza Mkuu wa Wilaya kwa maelekezo aliyoyatoa na kuahidi kumpa ushirikiano katika mapambano dhidi ya Ugonjwa wa CORONA.

“Tunampongeza Mkuu wa Wilaya hakika kikao hiki ni chakujenga kwa pamoja, ugonjwa huu unaua ndugu zetu wanateketea katika Mataifa mengine , kwahiyo tukuhakikishie Mkuu wetu wa Wilaya maagizo kwa pamoja tumeyapokea na tunakwenda kuyafanyia kazi , wote tukishirikiana kwa pamoja ugonjwa huu utakuwa ni historia kwetu wananchi wa Morogoro” Amesema Haule.



Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe. Regina Chonjo, akizungumza na Wananchi wa Stendi ya Daladala Mjini wakati wa zoezi la kuwakabidhi Ndoo pamoja na sabuni zilizotolewa na Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini, Mhe. Abdulaziz Abood kwa ajili ya kujikinga na Ugonjwa wa CORONA.



Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro akinawa maji wakati wa ukaguzi wa upuliziaji wa dawa za Corona katika Kituo cha Mabasi Msamvu.




*Afisa Ustawi Rehema Malimi akikabidhi ndoo katika Makao ya Watoto Dar-Ul- Muslimeen Kata ya Mbuyuni, zilizotolewa na Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro kwa ajili ya kujikinga na Virusi vya CORONA.*

# WANAWAKE WAJASIRIAMALI IBUENI MIRADI YENYE TIJA NA INAYOTEKELEZEKA ILI MUWEZE KUREJESHA MIKOPO KWA WAKATI-RAS MOROGORO.

INATOKA UK... 22

kwa vikundi 9 vya Wanawake, shilingi milioni 45,500,000.00/= kwa vikundi 11 vya Vijana na shilingi milioni 9,000,000.00/= kwa vikundi 3 vya watu wenye ulemavu.

Naye Afisa Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Morogoro, amesema katika mwaka wa fedha wa 2018/2019 , Halmashauri ya Manispaa Morogoro ilitoa mkopo wa Shilingi Milioni 402,500,000/= kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu ambapo vikundi 76 vya wanawake vilipatiwa mkopo wa shilingi milioni 214,500,000/=, vikundi 51 vijana walipewa shilingi milioni 151,500,000/= na vikundi 13 vya watu wenye ulemavu walipewa shilingi milioni 36,500,000/=.

Amesema mpaka kufikia Oktoba 2019 vikundi 22 vya wanawake vilipaswa viwe vimekamilisha marejesho , vikundi 12 pamoja na vikundi 11 vya watu wenye ulemavu vyote vilipaswa viwe vinaelekea katika kurejesha fedha.

Katika maadhimisho hayo miongoni mwa shughuli zilizokuwa zikifanyika ni pamoja na maonesho ya bidhaa mbalimbali za wanawake zinazofanywa na wajasiriamali pamoja na shughuli mbalimbali zinazofanywa na wadau , elimu ya jinsia na ukatili kwa wanafunzi wa shule za Msingi na Sekondari, huduma ya msaada wa kisheria kwa wananchi wenye uhitaji katika Kata ya Lukobe na Kata Jirani za Kihonda na Mkundi, Utoaji wa msaada kwa kituo kimoja cha watoto yatima kituo cha Mgolole, kambi ya Wazee Fungafunga, Gereza la wafungwa wanawake Kingolwira na kwa watoto wenye ulemavu wa akili kituo cha Mehayo Kata ya Mazimbu, Upimaji wa Saratani ya shingo ya kizazi na VVU , Bonanza kwa Wananchi wa Mzinga na uchangiaji wa damu salama pamoja na Mashindano ya michezo kwa wanawake ikiwemo kukimbiza kuku,



*Mkurugenzi Manispaa Morogoro Sheilla Likuba akikagua bidhaa za Wajasirimali wa ndani ya Manispaa katika Sherehe za maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani 8/3/2020.*

# SALAMU ZA MSTAHIKI MEYA WA MANISPAA YA MOROGORO MHE.PASCAL KIHANGA.

INATOKA UK... 24

za viwanja 8723 zimeandaliwa, sawa na asilimia 87.2 ya lengo la kuandaa hati miliki 2500 kila mwaka wa fedha. Aidha jumla ya mitaa 20 inaendelea na taratibu za Urasimishaji kwa lengo la kutekeleza Mkakati wa Urasimishaji Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA).Kazi urasimishaji inatekelezwa na zaidi ya makampuni na taasisi nane.

Kwa upande wa Manispaa sekta ya Mipango miji, Ardhi na Maliasili imeweza kuandaa michoro 152 ya mipango miji kwa kipindi cha 2015 - 2019. Aidha jumla ya viwanja 43,528 vilimilikishwa na idadi ya mashamba yaliyokuwa na miliki ni 133. Aidha takribani asilimia 20 ya mashamba hayo yamebadilishwa matumizi na kuwa viwanja vya matumizi mbalimbali.

Katika kipindi cha mwaka 2015 -2019 jumla ya viwanja 9768 vilipimwa kati ya malengo ya kupima viwanja 13000 sawa na asilimia 75 na serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi. Aidha jumla ya makazi 5,750 yamerasimishwa katika Mitaa 17 ndani ya Manispaa ya Morogoro.

Aidha kitengo cha Maliasili kimeweza kufanikisha zoezi la upandaji wa miti kutoka miti 2,214,000 hadi miti 3,295,000, watalii wanaotembelea vivutio mbalimbali ndani ya Manispaa wameongezeka kutoka 153 hadi 259, aidha vijana waongoza watalii wameongezeka kutoka 3 hadi sasa wamefika 5. Kwa upande wa ufugaji nyuki jumla ya mizinga 103 hadi 158 imeweza kutengenezwa na kumilikiwa na vikundi mbalimbali. Jumla ya klabu za mazingira za shule ya msingi kutoka 9 hadi 27 zimeanzishwa na za shule za sekondari kutoka 5 hadi 19 zimeanzishwa



*Milima ya uluguru ikionesha asili ya Mkoa wa Morogoro ambayo pia imekua ni moja ya vivutio vikubwa vya watalii Mkoani hapa*




***Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Sheilla Lukuba (kulia), akimkabidhi Mkuu wa Masijala ndoo na sabuni iliyotolewa na Meya wa Manispaa ya Morogoro, Mhe. Pascal Kihanga kwa ajili ya kujikinga na Ugonjwa wa CORONA.***

# AUTI YA MANISPAA MOROGORO










# JARIDA LA MWEZI

Toleo namba 02

Mwezi Januari - Machi 2020



**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO**


OFISI YA MKURUGENZI
S.L.P 166
**MOROGORO TANZANIA**



(C) 2020